# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## OFISI YA RAIS -TAMISEMI
### HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA.

MAWASILIANO:
***0754629287/0621932547***
***Email:mataba2007@gmail.co***,

Shule ya Sekondari Mataba,
S.L.P.372,
**MASWA.**

Kumb Na: MTSS/JOIN/V/20 01/12/2020

---

JINA LA MWANAFUNZI: ………………………………………………………………………………
S.L.P………………
**………………………….**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MATABA WILAYA YA MASWA MKOA WA SIMIYU MWAKA 2021.**

**1.0. UTANGULIZI:**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechugliwa kujiunga na **kidato cha kwanza** katika shule hii **mwaka 2021**.

Shule itafunguliwa kwa muhula wa kwanza tarehe **11.01.2021** siku ya **JUMATATU** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11.01.2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18.01.2021** ndani ya siku saba (7).

**2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.**

**2.1. Sare za shule**

(a) **Wavulana:** Suruali (2) rangi ya **kaki** kitambaa cha suti ikiwa na marinda mawili (2), shati mbili (2) nyeupe tetron mikono mifupi.

❖ **Wasichana:** Sketi mbili (2) **moja rangi ya kaki na nyingine rangi ya zambarau** kitambaa cha Suti zikiwa na mshono wa Rinda Box ndefu zikiwa juu ya kifundo cha mguu , na shati mbili (2) nyeupe Tetron mikono mifupi.

(b) Rangi ya Hijabu ifanane na sare za shule.
   (i) **Sare ya michezo**: Bukta blue na T-shirt rangi ya nyekundu kwa wavulana na wasichana ziwe na nembo ya shule na ni kwa ajili ya michezo tu.
   (ii) Raba kwa ajili ya michezo.

(c) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika visivyo na kisigino kirefu au soli nene na soksi jozi mbili (2) kwa wavulana na viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika visivyo na kisigino kirefu na soksi ndefu jozi mbili (2) “Stocking” kwa wasichana.

**2.2. Mahitaji mengine.**

1. Daftari kubwa kumi na moja (Counter book) 11.
2. Kalamu za wino na penseli
3. Mkebe wa hesabu.
4. Mfuko wa kubebea daftari (school bag).
5. Faili moja (1) kwa ajili ya kuhifadhia taarifa zako.

## 3.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu **Na. 25** ya mwaka **1978** na kama ilivyorekebishwa kwa **Sheria Na. 10** ya mwaka **1995**. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi,teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.


a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya Shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wowote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
i) Kutunza mali za umma.

## 4.0. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

(a) Wizi.
(b) Uasherati na ushoga
(c) Ubakaji
(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
(e) Kupigana / kupiga.
(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
(g) Kudharau Bendera ya Taifa.
(h) Kuwa mjamzito / kupata mimba
(i) Kuoa au kuolewa
(j) Kutoa mimba
(k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
(l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
(m) Kuwa na simu ya mkononi.

"KARIBU SANA MATABA SEKONDARI"






**Iddi O. Lameck**
**MKUU WA SHULE**

# OFISI YA RAIS -TAMISEMI

## MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI NA MKATABA WA KUFUATA SHERIA ZA SHULE.

1. Jina la Mwanafunzi ...........................................................................
2. Tarehe ya kuzaliwa: ............................
3. Shule ya Msingi:............................................... Namba ya Mtihani ........................
   Kata ya ........................................... Tarafa .....................................
4. Jina kamili la baba: ..........................................................................Hai/amefariki
   Kijiji ...................................... Kata ............................. Tarafa …........................
5. Jina kamili la Mama: ......................................................................... Hai / amefariki
   Kijiji ...................................... kata ............................. Tarafa .........................
6. Jina kamili la mlezi (kama hana mzazi) ......................................................................
7. Uhusiano na mlezi ..................................................................................................
8. Kazi ya Baba / Mlezi ...............................................................................................
9. Jamaa katika familia:-
   (a) Idadi ya kaka ......................................
   (b) Idadi ya dada ......................................
   (c) Yeye ni wa ngapi katika familia ........................

**NB**: Nathibitisha kuwa nimesoma na kuelewa vizuri sheria za shule hii na kwamba nathibitisha kuwa sitashiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

Ee Mungu nisaidie.

...................................

……………………………………………………………………….

**Sahihi na jina la Mwanafunzi.**

# PRESIDENTS' OFFICE, -TAMISEMI

MATABA SEC. SCHOOL,
P.O BOX 357,
**MASWA.**

DATE: ........................

TO THE MEDICAL OFFICER,
..........................................
.........................................
..........................................

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION.**

Please examine the above mentioned girl/boy as to her/his fitness for studies in this school. (This form must be completed by Government Medical Officer).

Student's full name: ..........................................................................................
Present age: ..........................................................................................
Blood test: ..........................................................................................
Stool examination: ..........................................................................................
TS test: ..........................................................................................
Asthma: ..........................................................................................
Eye Disorder: ..........................................................................................
Nose Disorder: ..........................................................................................
Skin Diseases: ..........................................................................................
Anemia: ..........................................................................................
Chest: ..........................................................................................
Operations: ..........................................................................................
Serious accidents: ..........................................................................................
Any other infections / diseases: ......................................................................
Pregnancy……………………………………………………………………………

**ADDITIONAL INFORMATION E.g. Physical defects or impairment.**

..........................................................................................................
..........................................................................................................

I certify that I have personally examined Mr./Miss .......................................... and found him/ her fit to pursue his / her studies.

Signature: ............................................ Designation: ...........................

Official stamp: ..................................